

## Utangulizi wa Isimu Jamii - Isimu Jamii Notes

- [Utangulizi](#)
- [Mambo Yanayoshughulikiwa Katika Isimu Jamii](#)
- [Umuhimu wa Isimu Jamii](#)
- [Maana ya Mawasiliano](#)
  - [Njia Ambazo Kwazo Mwanadamu Huwasiliana](#)
- [Lugha](#)
  - [Sifa za Lugha](#)
  - [Sababu za Kufa/Kufifia kwa Lugha.](#)
  - [Umuhimu wa Lugha](#)
- [Istilahi za Isimu Jamii](#)
  - [Isimu \(linguistics\)](#)
  - [Lugha](#)
  - [Sajili](#)
  - [Fonolojia](#)
  - [Fonetiki](#)
  - [Mofolojia \(au sarufi maumbo\)](#)
  - [Sintaksi \(au sarufi miundo\)](#)
  - [Semantiki](#)
  - [Diglosia](#)
  - [Polyglosia](#)
- [Aina za Lugha Katika Isimu Jamii](#)
  - [Lafudhi](#)
  - [Lahaja](#)
  - [Lugha rasmi](#)
  - [Lugha rasimi](#)
  - [Lugha ya taifa](#)
  - [Lugha Sanifu](#)
  - [Lingua Franka](#)
  - [Pijini](#)
  - [Krioli](#)
  - [Lugha mame](#)
  - [Lugha azali](#)
  - [Misimu](#)
  - [Uwili lugha](#)
  - [Tofauti Kati ya Kuchanganya Ndimi na Kuhamisha Ndimi](#)
  - [Sababu za kuchanganya na kuhamisha ndimi](#)
- [Kaida katika jamii ambazo matumizi ya lugha hutegemea](#)
  - [Mazingira/muktadha](#)
  - [Umri](#)
  - [Uhusiano](#)
  - [Jinsia/uana](#)
  - [Madhumuni/lengo](#)
  - [Mada](#)
  - [Hali ya mtu](#)
  - [Cheo cha mtu/hadhi](#)
  - [Utabaka](#)

## Utangulizi

Isimu Jamii (social linguistics) - ni tawi la isimu (elimu ya lugha) linalochunguza namna lugha inavyotumika katika jamii na uhusiano baina yake. Tawi hili huzingatia matumizi ya lugha katika mazingira tofauti; aina mbali mbali za lugha na mazingira yake; uhusiano kati ya lugha na utamaduni wa jamii inayoitumia.

Isimu- ni uchunguzi wa lugha kisayansi.

Jamii - ni kundi filani la watu wenye uhusiano fulani.

## Mambo Yanayoshughulikiwa Katika Isimu Jamii

- i. Tofauti katika lahaja za lugha kama vile Kiswahili cha lamu(kiamu), cha Mombasa(kimvita), cha unguja(kiunguja), cha bara.
- ii. Tofauti katika matumizi ya lugha baina ya makundi tofauti tofauti katika jamii. Mfano wazee na watoto, vijana na wabunge.
- iii. Matumizi ya lugha kutegemea miktadha tofauti kama vile kazini, nyumbani, sokoni, n.k.
- iv. Mtazamo wa watu kuhusu lugha. Je, wanaitukuza au wanaitweza?
- v. Jinsi mtu anavyotumia lugha kutegemea uhusiano na wazungumzaji au mada husika.
- vi. Lahaja mbalimbali za lugha ya Kiswahili.

## Umuhimu wa Isimu Jamii

- i. Huwafunza watu kaida za lugha ili waweze kuitumia ipasavyo kutegemea mila na desturi.
- ii. Humsaidia mzungumzaji au mwandishi kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na usahihi.
- iii. Humpa anayetumia lugha uwezo wa kutambua, kutofautisha na kutumia mitindo mbalimbali ya lugha kutegemea mahitaji.
- iv. Hufunza maadili ya jamii hasa yanayohusiana na matumizi ya lugha kutegemea uhusiano. Mf. Mtu na mkwewe, mtoto na mzazi, mwajiri na mwajiriwa.
- v. Hufunza mbinu za mawasiliano pamoja na mbinu za kupata maana kamili.
- vi. Hudhihirisha utamaduni wa jamii.
- vii. Humsaidia msemaji au mwandishi kutambua makosa mbalimbali yanayojitokeza wakati wa kuzungumza au kuandika.
- viii. Hufunza mbinu za kuwaelewa watu tunaotagusana

## Maana ya Mawasiliano

Utaratibu ambao huwawezesha viumbe kupashana ujumbe ambao unahusisha mwasilishi na mpokeaji wa ujumbe.

## Njia Ambazo Kwazo Mwanadamu Huwasiliana

- i. Mgusano na ukaribianaji
- ii. Mavazi
- iii. Sauti
- iv. Ishara za mwili.

## Lugha

Ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa na wanadamu katika mawasiliano.